


Mungu hakudhanii hivyo. Mungu anakuona kuwa kiumbe muhimu sana katika ulimwengu hata akamtuma mwanawe Yesu Kristo kufa badala yako. Ikiwa umeamua kumwamini Yesu Kristo kuwa mwokozi wako, mbona usitumie nafasi hii kumshukuru kwa kukuthamini na kumuomba aingie moyoni mwako. Hakikisha maombi yako ni ya dhati kutoka kwa moyo uliovunjika mbele ya Bwana. Ikiwa kijitabu hiki kimekusaidia kumwamini Yesu Kristo kama mwokozi wa maisha yako, tafadhali tuandikie ili tusherekee pamoja nawe.

 **HopeTractMinistry**
of Bethel Baptist Church

P.O. BOX 1115 • YORK, SC 29745 • 803-684-1535
WWW.HOPETRACTS.ORG

What Is The Most Important Thing? (Swahili) Tract 505



**NINI KILICHO MUHIMU
ZAIDI YA VYOTE
ULIMWENGUNI?**

Je, umewahi kutambua kitu ambacho Mungu hudhania kuwa muhimu zaidi ya vyote ulimwenguni? Je, ni dhahabu na fedha, utajiri wa walimwengu, uzuri wa mahali mbalimbali, utu wema wa watu, au werevu na sherehe za wanasiasa? Ama ni hekima ya wanasayansi, unenaji wa wanenaji wema, au ni majumba na kumbi za vyo vya wasomi? Kwa kweli, si kati ya hivi vitu vyote.

Ni kweli kwamba *“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe nauzima wa milele.”* Yohana Mtakatifu 3:16. Na ni kweli kwamba *“Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.”* (Luka Mtakatifu 19:10) Vile vile *“kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.”*

(Warumi 3:23). Mungu asema pia *“Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa mwenye dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate haki ya Mungu katika Yeye.”* 2 Wakorintho 5:21. Kitu kilicho muhimu sana kwake Mungu ulimwenguni zaidi ya vyote ni binadamu. Kwa hivyo ni mapenzi yake Mungu injili yake Yesu Kristo ihubiriwe kwa kila mwanamume na mwanamke, kila mvulana na mschana ulimwenguni. Mungu amekuwezeshwa kusoma kijitabu hiki ili uelewe mpango wake kwa maisha yako.

Rafiki mpendwa, *“Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanvyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.”* (Waraka wa pili wa Petro 3:9)

Wewe u muhimu sana mbele za Mungu. Mungu pekee ndiye ajuaye uzuri wa mbinguni na mateso ya kuzimu. Mungu pekee ndiye awezaye kutuokoa kutoka kuzimu na kutupeleka mbinguni. Usimruhusu mtu yeyote kuyadharau maisha yako maana Mungu anayathamini sana. *“Kwa kuwa itamfaidi mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?”* (Marko Mtakatifu 8:36,37).

Mungu anakuthamini sana. Amekutolea kila ambacho angeweza kutoa ili upate nafasi ya kuishi milele mbinguni.

Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 1:12 *“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wakufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;”* Je, utampokea Yesu?

Yesu alisema pia katika Mathayo Mtakatifu 11: 28 *“Njoni kwangu, nyinyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.”* Tumeambiwa katika Warumi 10:9,13 *“Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa kuwa, Kila atakayeliita Jina la Bwana ataokoka.”* Je, utaamini moyoni mwako kwamba Mungu alituma Yesu Kristo kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako, alizikwa na akafufuka kutuhesabia haki. Je, u tayari kutoa ushuhuda juu ya imani yako katika Kristo Yesu? Kama umejitolea kuyazingatia haya Mungu asema umeokoka. Kuna wengi ambao hujidharau kuwa si kitu duniani.